**MUHTASARI WA KIKAO MAALUM CHA MENEJIMENTI KILICHOFANYIKA TAREHE 25/10/2021 KWENYE UKUMBI WA OFISI KUU YA JIJI LA TANGA.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg. Sipora Liana | Mkurugenzi wa Jiji | M/kiti |
| 2. | Ndg. Rehema Mwakuro | Kaimu Mkuu wa Idara ya Utawala na Katibu Rasilimali Watu | |
| 3. | Ndg. Simon Mdende | Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii | Mjumbe |
| 4. | Ndg. Edward P. Barigira | Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA | " |
| 5. | TP. Antelius Anglibert | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipangomiji, Maliasili na Mazingira | " |
| 6. | Eng. Arafat Kaniki | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi | " |
| 7. | Ndg. Kizito L. Nkwabi | Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira | " |
| 8. | Ndg. Hawa Msuya | Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika | " |
| 9. | Ndg. Simeon Vedastus | Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji | " |
| 10. | Ndg. Gwakisa Lusajo | Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondar | " |
| 11. | Ndg. Fatuma Nkya | Kaimu Mkuu wa idara ya elimu msingi | " |
| 12. | Dr. Gideon Joshua | Kaimu Mkuu wa Idara ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe | " |
| 13. | Adv. Sebastian Danda | Mkuu wa Kitengo cha Sheria | " |
| 14. | CPA.Jemima Japhet | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani | " |
| 15. | Ndg. Lucia Marandu | Afisa Biashara. | " |
| 16. | Ndg. Mussa Labani | Kaimu Afisa Habari na Uhusiano | " |
| 17. | Ndg. Juma Mkombozi | Mratibu wa TASAF | " |
| 18. | Ndg. Cornery Sima | Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara | " |
| 19. | Dkt. Paul Kisaka | Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi | " |
| 20. | Ndg. Leonard Sembe | Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya | " |
| 21. | Ndg. Mustin Mustapher | Mhasibu wa Mapato. | " |
| 22. | SP. Sophia Lydenge | Msimamizi wa Polisi Wasaidizi | |



CamScanner

**SEKRETARIETI:**

1. Ndg. Ismail S. Mtomaye — Afisa Utumishi
2. Ndg. Abbas B. Kabwe — Katibu kamati
3. Ndg. Perpetua Mhina — Afisa Utumishi

**MUHT/TCC/CMT/NA 83: 2021/2022. KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alianza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu. Kisha aliwataka wajumbe kutoa ushirikiano katika kujadili agenda za kikao. Baada ya maelezo hayo Mwenyekiti alifungua kikao saa 03:57 Asubuhi.

**MUHT/TCC/CMT/NA 84: 2021/2022. KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO**

Agenda zifuatazo zilisomwa mbele ya wajumbe na kwa kauli moja waliridhia zijadiliwe.

1. Kufungua kikao.
2. Kuthibitisha agenda za kikao.
3. Mapokezi ya Fedha Tshs. 1,160,000,000.00 za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya Uviko-19 na Ombi la idhini ya Kufanya Uhamisho wa nje (Reallocation Between) wa Fedha zilizopokelewa.
4. Kufunga kikao.

**MUHT/TCC/CMT/NA85: 2021/2022. MAPOKEZI YA FEDHA TZS. 1,160,000,000.00 ZA MPANGO WA MAENDELEO KWA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO-19 NA OMBI LA IDHINI YA KUFANYA UHAMISHO WA NJE (REALLOCATION BETWEEN) WA FEDHA ZILIZOPOKELEWA.**

Ilielezwa kuwa Halmashauri ya Jiji la Tanga imepokea fedha katika akaunti za shule za sekondari kiasi cha shilingi 1,080,000000.00 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 54. Fedha hizi ni Mkopo Nafuu toka Shirika la Fedha Duniani (IMF) ukiwa na lengo la kuwezesha kuboresha maeneo ya kujifunzia wanafunzi ili kupambana na maambukizo ya UVIKO-19. Shule zilizopatiwa fedha hizo ni kama zinavyoonekana katika jedwali;

**Ujenzi wa madarasa 54 kwa shule za sekondari - Mkopo Nafuu IMF**

| NA | FEDHA ZILIZOPOKELEWA | MIUNDOMBINU YA UJENZI |
|---|---|---|
| 1 | 60,000,000.00 | Ujenzi wa vyumba 03 vya madarasa shule ya sekondari Mwapachu |

| | | |
|---|---|---|
| 2 | 40,000,000.00 | Ujenzi wa vyumba 02 vya madarasa shule ya sekondari Maweni |
| 3 | 200,000,000.00 | Ujenzi wa vyumba 10 vya madarasa shule ya sekondari Pongwe |
| 4 | 60,000,000.00 | Ujenzi wa vyumba 03 vya madarasa shule ya sekondari Mikanjuni |
| 5 | 40,000,000.00 | Ujenzi wa vyumba 04 vya madarasa shule ya sekondari Pande Magubeni |
| 6 | 280,000,000.00 | Ujenzi wa vyumba 14 vya madarasa shule ya sekondari Saruji |
| 7 | 10,000,000.00 | Ujenzi wa vyumba 05 vya madarasa shule ya sekondari Chumbageni |
| 8 | 60,000,000.00 | Ujenzi wa vyumba 03 vya madarasa shule ya sekondari Japan |
| 9 | 60,000,000.00 | Ujenzi wa vyumba 03 vya madarasa shule ya sekondari Horten |
| 10 | 60,000,000.00 | Ujenzi wa vyumba 03 vya madarasa shule ya sekondari Msambweni |
| 11 | 40,000,000.00 | Ujenzi wa vyumba 04 vya madarasa shule ya sekondari Kihere |
| | **1,080,000,000.00** | |

Ilielezwa kuwa zimepokelewa fedha zingine katika akaunti ya shule ya msingi Chuda kiasi cha shilingi 80,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa bweni la wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa lengo la kuendelea kupambana na maambukizi ya UVIKO-19.

Ilielezwa kuwa Pamoja na mapokezi ya fedha hizi ninaomba kikao chako kiridhie fedha hizi kuombewa uhamisho wa nje (Reallocation Between) kwa sababu zipo nje ya bajeti ya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na kuridhia pia taarifa hii kuwasilishwa katika kikao cha Kamati ya Fedha na Uongozi ili kupata ridhaa ya kikao kwa ombi la mapendekezo ya kufanyika kwa uhamisho wa nje liweze kuwasilishwa kwa Katibu Tawala Mkoa kwa hatua zaidi. Aidha Utekelezaji wa mradi huu kwa mujibu wa maelekezo imeruhusiwa kutumika njia ya "Force Account", kutumia Mkandarasi au Single Source lakini kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo inayosimamia njia hizo za manunuzi.

**Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuijadili kama ifuatavyo.**

**i. Muda wa Utekelezaji wa Mradi.**

Wajumbe walisisitiza wahusika wahakikishe wanazingatia muda wa utekelezaji wa miradi husika ili ifikapo mwezi Januari 2022 madarasa hayo yaanze kutumika.

Ilielezwa kuwa ushauri wa wajumbe umezingatiwa.

**i. Ubora wa Miradi ya Ujenzi.**



CS CamScanner

Wajumbe walisisitiza wahandisi na wasimamizi wengine wahakikishe wanazingatia ubora wa miradi iendane na thamani ya fedha ili miradi hiyo iwe na tija iliyokusudiwa. Ilielezwa kuwa ushauri wa wajumbe umezingatiwa.

**Baada ya majadiliano hayo wajumbe waliipitisha taarifa hiyo na kuridhia mchakato wake uendelee.**

**MUHT /TCC/CMT/NA. 86.2021/2022: KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa ushirikiano wao walioutoa katika muda wote wa kikao. Baada ya maelezo hayo Mwenyekiti alifunga kikao saa 04.49 Asubuhi.

**UMETHIBITISHWA**

| | | |
|---|---|---|
| ....................................... | | ....................................... |
| **KATIBU** | 19/11/2021 | **MWENYEKITI** |
| | **TAREHE** | |